**JIMBO LA VERMONT**

**MAHAKAMA KUU** **IDARA YA KIRAIA**

Kitengo Nambari ya Doketi.

| Mlalamikaji | TAREHE YA KUZALIWA | Mshtakiwa | TAREHE YA KUZALIWA |
|---|---|---|---|
| | | | |

# NIA YA KUENDELEA KUFUATILIA AU KUONDOA MALALAMIKO

## Unyemeleaji

## KULINGANA NA 12 V.S.A. §5133

**Teua Kisanduku Kinachofaa**

☐ Ninaelewa kuwa ombi langu la msaada wa dharura limekataliwa. Ninaondoa ombi langu la amri ya mwisho dhidi ya unyemeleaji inayotafutwa chini ya 12 V.S.A. §5133.

**AU**

☐ Licha ya ukweli kwamba ombi langu la msaada wa dharura lilikataliwa, ninakusudia kuendelea kufuatilia ombi langu la amri ya mwisho dhidi ya amri ya unyemeleaji chini ya 12 V.S.A. §5133. Naomba usikilizaji upangwe.

Saini ya Mlalamikaji ______________________________ Tarehe ______________________

## NOTISI MUHIMU
## NIA YA KUENDELELEA KUFUATILIA AU KUONDOA MALALAMIKO KWA AMRI YA ULINZI DHIDI YA UNYEMELEAJI

### MAELEZO MUHIMU KWA MLALAMIKAJI

**Ikiwa hakuna ombi la usikilizaji lililowasilishwa ndani ya siku tano (5) za kazi tangu tarehe ya amri ya kukataliwa ilipotolewa, ombi la amri ya mwisho litazingatiwa kuwa limeondolewa.**

### MAELEZO KWA MLALAMIKAJI NA MSHTAKIWA KUHUSU UWAKILISHWAJI NA MWANASHERIA

**Ingawa unaweza kujiwakilisha mwenyewe katika usikilizaji wowote wa kesi wakati wa kesi hizi, unaweza kutaka kushauriana na au kuwakilishwa na mwanasheria. Ukimkodi mwanasheria kukuwakilisha, mwanasheria wako anatakiwa kuijulisha Mahakama na upande mwingine kwamba atakuwakilisha. Pande zote mbili zina haki ya kupokea "notisi" kabla ya usikilizaji wowote kwamba upande pinzani utawakilishwa na mwanasheria. Sheria za Vermont za Taratibu za Kesi za Kiraia zinahitaji kwamba notisi kama hiyo lazima itolewe kwa upande pinzani au mwanasheria wao ana kwa ana, kwa simu, au kwa maandishi na lazima itolewe kwa muda wa kutosha kabla ya usikilizaji ili kuwaruhusu kuwa na mwanasheria pia. Usipotoa notisi hiyo kwa upande pinzani, na ikiwa upande usio na mwanasheria utaomba, Mahakama itaahirisha usikilizaji kwa muda unaofaa ili kuruhusu upande usio na uwakilishi kupata mwanasheria.**

### MAELEZO MUHIMU KWA MSHTAKIWA

**Katika usikilizaji utakaofanyika tarehe na saa zilizotajwa kwenye upande wa mbele wa notisi hii, Mahakama itaamua kama itatoa au kukataa kutoa amri ya mwisho. Baada ya usikilizaji, amri inaweza kutolewa, ambayo inaweza kutumika kwa muda uliowekwa, ambao utatajwa kwenye amri. Ukikosa kufika kwenye kikao cha usikilizaji, amri inaweza kutolewa dhidi yako kwa kukubali maombi ya Mlalamikaji ya kupata msaada kadri Mahakama itakavyoona inafaa.**

# UTHIBITISHAJI WA UTOAJI WA HUDUMA

## JIMBO LA VERMONT

**MAHAKAMA KUU** **IDARA**

**Kitengo** **Nambari ya Doketi.**

Nilipeleka mwenyewe: (teua zote zinazohusika)

- ☐ Malalamiko, Hati ya Kiapo na Amri ya Muda
- ☐ Amri ya Muda
- ☐ Amri ya Mwisho
- ☐ Hati ya Maelezo ya Huduma ya Mahakama
- ☐ Amri ya Muda Iliyobadilishwa/Iliyorekebishwa
- ☐ Amri ya Mwisho Iliyobadilishwa/Iliyorekebishwa
- ☐ Amri ya Kurekebisha/Kuongeza/Kuondoa Amri
- ☐ Amri ya Mwisho Iliyoongezwa muda
- ☐ Amri ya Muda Iliyoongezwa muda
- ☐ Kunyimwa Msaada wa Dharura
  Nia ya Kuendelea Kufuatilia
  Notisi ya usikilizaji

Mnamo ______________________________ na: ______________________________

Tarehe: ______________ Saa: ______________ ☐ ASB ☐ MCH Mahali: ______________________________

| Tarehe | Jina la Afisa, Cheo na Wakala | Saini ya Afisa |
|---|---|---|
| | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Uthibitisho wa Kupokea Huduma** | |
| | | Ninakubali kuwa nimepokea huduma kuhusiana na amri hili. | |
| **Ada** | | Tarehe | Saini |
| Ada ya Huduma | | | |
| Maili ____ **X** $0. _____ kwa kila maili | | (tafadhali chapisha au andika jina) | |
| Jumla | | | |